*Mulika, Na. 42 (1), 83-103*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uchanganuzi wa Tungo zenye Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili: Sifa za Muundo wa Taarifa na Sababu za Upinduzi wa Kimahali katika Mawasiliano

*Fabiola Hassan*[1]
Chuo Kikuu cha Dodoma

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na42t1.6

**Ikisiri**

Kuna uhusiano baina ya udarajia wa dhima za kisemantiki na dhima za kisarufi. Uhusiano uliopo ni kwamba kiambajengo kilichopo katika nafasi ya juu katika udarajia huo ndicho kinapaswa kuwa kiima na sio kiambajengo kilichopo katika nafsi ya chini. Tungo zenye upinduzi wa kimahali zinakiuka uhusiano huo. Katika tungo hizo, kimahali, ambacho kipo katika nafasi ya chini, kinakuwa kiima ilihali sio mtenda au kithimu. Wataalamu mbalimbali wamefafanua tungo hizi katika lugha za Kibantu. Licha ya kufanya hivyo, hakuna uwazi kuhusu sifa za muundo wa taarifa na sababu za upinduzi wa kimahali katika mawasiliano. Hivyo, makala haya yanafafanua na kubainisha masuala hayo katika lugha ya Kiswahili. Data zilizotumika zimepatikana kwa mbinu ya uchambuzi wa matini, upimaji wa usahihi wa kisarufi pamoja na usaili. Data hizo zimefasiriwa kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu (Bresnan na Kaplan, 1982). Baada ya kufasiri data hizo, makala haya yanabainisha kwamba muundo wa taarifa wa tungo hizi una aina mbili za taarifa, yaani mada na fokasi. Aidha, makala yanafafanua kwamba upinduzi wa kimahali unatokea kwa sababu ya umadaishaji wa kimahali na ufokalishaji wa kithimu/mtenda.

## Utangulizi

Tungo yenye upinduzi wa kimahali ni tungo ambayo, kwayo, kiambajengo kinachorejelea mahali (kimahali), ambacho kwa kawaida hutokea baada ya kitenzi, hupandishwa hadhi na kuhamishwa nafasi kwenda katika nafasi ya kiima. Wakati huohuo, kiambajengo kinachorejelea kithimu au mtenda, ambacho kwa kawaida hutokea kabla ya kitenzi katika nafasi ya kiima, hushushwa hadhi na kuhamishwa nafasi kwenda baada ya kitenzi. Mfano Na. 1 (b) unaonesha tungo yenye upinduzi kimahali katika lugha ya Kiswahili:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1(a) | *Taka* | *zi-me-zaga-a* | ***sakafu-ni*** |
| | kng10.taka | kk10-knj-zaga-kt | kng9.sakafu-ktm |
| | 'Taka zimezagaa sakafuni .' | | |

[1] Baruapepe: fabiolahassan0@gmail.com

| | | | |
|---|---|---|---|
| (b) | ***Sakafu-ni*** | *pa-me-zaga-a* | *taka* |
| | kng7-kng9.sakafu-ktm | kng16-knj-zaga-ktm | kng10.taka |

‘Sakafuni pamezagaa taka.’

Mfano Na. 1 (a) unaonesha tungo isiyo na upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, kimahali *sakafuni* kipo baada ya kitenzi *zimezagaa* na kithimu *taka* kipo kabla ya kitenzi hicho katika nafasi ya kiima. Mfano Na. 1 (b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, kimahali *sakafuni* kimepandishwa hadhi na kutokea kabla ya kitenzi *pamezagaa* na kithimu *taka* kimeshushwa hadhi na kutokea baada ya kitenzi hicho.

Katika lugha za Kibantu, tungo zenye upinduzi wa kimahali zinakiuka kanuni ya uhusiano wa udarajia wa dhima za kisemantiki na dhima za kisarufi za viambajengo vya sentensi. Udarajia wa dhima za kisemantiki ni mpangilio wa dhima za kisemantiki kwa kuzingatia uwezekano wa dhima husika kuwa kiima (Dowty, 1991). Kwa kawaida, kanuni inadai kwamba, kiambajengo chenye dhima iliyopo katika nafasi ya juu, yaani upande wa kushoto zaidi, ndicho kinapaswa kuwa kiima kuliko kiambajengo chenye dhima iliyopo katika nafasi ya chini, yaani upande wa kulia. Wanaisimu wamependekeza udarajia wa dhima za kisemantiki katika lugha za Kibantu (Baker; 1989; Bresnan na Kanerva, 1989; na Mkude, 2005). Katika darajia mbalimbali zilizopendekezwa, kimahali kinatokea katika nafasi ya chini kuliko mtenda na kithimu. Kielelezo Na. (1) kinaonesha udarajia wa dhima za kisemantiki:

**Kielelelezo Na. (1): Udarajia wa Dhima za Kisemantiki katika Lugha za Kibantu**

*Mtenda > Mnufaika >Mpokeaji/Mhisi > Kithimu/Kiathirika > Ala > Kimahali*

**Chanzo**: Bresnan na Kanerva (1989: 25)

Kielelezo Na. (1) kinaonesha udarajia wa dhima za kisemantiki katika lugha za Kibantu. Katika udarajia huu, kimahali kinatokea katika nafasi ya chini kabisa kuliko mtenda, mnufaika, mpokeaji/mhisi, kithimu/kiathirika. Licha ya kwamba kimahali kinatokea katika nafasi ya chini; katika tungo zenye upinduzi wa kimahali, kinapandishwa hadhi na kuwa kiima hata kama kuna mtenda au kithimu. Kwa mfano, katika data Na. 1 (b), tunaona kimahali *sakafuni* kimepandishwa hadhi na kuwa kiima ingawa katika tungo hiyohiyo kuna kithimu *taka*. Hivyo, tungo zenye upinduzi wa kimahali zinakiuka uhusiano wa udarajia wa dhima za kisemantiki na za Kisarufi.

Wamaisimu mbalimbali wamefanya tafiti kuhusu tungo hizi katika lugha zisizo za Kibantu pamoja na lugha za Kibantu, kikiwamo Kiswahili. Kwa mfano, Bresnan (1990) na Her (2003; 2006) wamefanya tafiti kuhusu tungo hizi katika lugha zisizo za Kibantu ambazo ni Kiingereza na Kichina, mtawalia. Pia, Bresnan na Kanerva

(1989), Demuth na Mmusi (1997), Salzman (2004), Marten (2006), Buel (2007), Diercks (2009), Creissels (2011), Zeller (2013) pamoja na Marten na van Der Wall (2014) wamefanya tafiti kuhusu tungo hizi katika lugha za Kibantu. Aidha, Krifka (1959), Mkude (2005), Marten (2013), Marten na van der Wal (2014), Hassan (2018) na Hassan (2019) wamechunguza tungo hizi katika lugha ya Kiswahili. Wanaisimu hawa waliotangulia, wameeleza masuala mbalimbali kama vile aina za tungo zenye upinduzi wa kimahali, vitenzi vinavyoruhusu na visivyoruhusu utokeaji wa tungo hizi pamoja na dhima za kisarufi za viambajengo vinavyohusika katika tungo hizi. Kwa mfano, Marten (2013) anaeleza kwamba, katika lugha ya Kiswahili, kimahali kilichopinduliwa kina dhima ya kiima kwa sababu ndicho kinachoukilia upatanishi wa kisarufi baina ya kimahali na kitenzi. Hassan (2018) anaeleza kwamba kuna aina mbili za tungo zenye upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili. Aina hizo ni tungo zenye upinduzi wa kimahali wa kimofolojia na zile zenye upinduzi wa kimahali wa kisemantiki. Anaeleza pia kwamba, vipo vitenzi vinavyoruhusu na vile ambavyo haviruhusu utokeaji wa tungo hizi. Pia, anafafanua kuhusu vimahali vinavyoweza kupinduliwa na vile visivyoweza kupinduliwa katika tungo. Naye, Hassan (2019) anafafanua kuhusu dhima za kisarufi za viambajengo vinavyohusika katika tungo zenye upinduzi wa kimahali ikilinganishwa na zile zisizo na upinduzi wa kimahali. Licha ya wataalamu waliotangulia kueleza masuala mengi, bado kuna masuala ya msingi ambayo hayajaelezwa kuhusu tungo hizi ambazo zinakiuka kanuni ya uhusiano wa udarajia wa dhima za kisemantiki na za Kisarufi. Miongoni mwa masuala ambayo hayajawekwa wazi ni muundo wa taarifa wa tungo hizi pamoja na sababu za matumizi yake katika mawasiliano ya wanalugha. Kinyume na watafiti waliotangulia, makala haya yanabainisha sifa za muundo wa taarifa katika tungo hizi. Pia, makala yanafafanua sababu za upinduzi wa kimahali katika mawasiliano ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Ili kufikia malengo haya, utafiti uliozaa makala haya umetumia mbinu mbalimbali za utafiti kama inavyofafanuliwa katika sehemu inayofuata, yaani sehemu 2.0.

**1.0 Mbinu za Utafiti Zilizotumika**

Utafiti uliozaa makala haya ulifanyika katika maeneo mawili. Maeneo hayo ni Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu iliyo katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na Idara ya Lugha ya Kiswahili, Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Maeneo haya yanapatikana katika vyuo vikuu vikongwe kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar ambapo mtafiti aliweza kupata matini zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Pia, aliweza kuwapata watoataarifa (wanafunzi na wahadhiri wa Kiswahili) ambao wana umilisi na ujuzi kuhusu kanuni za matumizi ya lugha ya Kiswahili, lugha ambayo inatumika katika mawasiliano rasmi ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Kuhusu sampuli, mtafiti alitumia vitabu vitatu Ashon (1944), Whiteley (1968) na Vitale (1977) pamoja na watoataarifa 10. Matini na watoataarifa waliotumika walipatikana kwa mbinu ya usampulishaji

lengwa, yaani mtafiti alilenga matini zilizoandikwa kuhusu Kiswahili na zenye tungo nyingi zenye upinduzi wa kimahali. Pia, aliwalenga wahadhiri na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu ambao wanafanya mawasiliano yao ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia Kiswahili sanifu. Ili kuwapata watoataarifa 10 pamoja na vitabu vitatu , mtafiti alitumia usampulishaji nasibu ulorahisi.

Data zilizotumika katika makala haya zilipatikana kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini, upimaji wa usahihi wa kisarufi pamoja na usaili. Katika mbinu ya uchambuzi wa matini, mtafiti aliandaa mwongozo wa uchambuzi wa matini kwa kuzingatia malengo ya utafiti na matini alizosoma. Mwongozo huo uliongoza kupata tungo zenye upinduzi wa kimahali ili kubaini sifa za muundo wake wa taarifa pamoja na sababu za upinduzi wa kimahali katika mawasiliano. Hivyo, mtafiti alisoma vitabu vitatu ambavyo ni Ashton (1944), Whiteley (1968) na Vitale (1977). Kwa kutumia mwongozo alioaundaa, alikusanya tungo zenye upinduzi wa kimahali kutoka kwenye vitabu hivyo vitatu ambavyo ni Ashton (1944), Whiteley (1968) na Vitale (1977). Tungo hizo ndizo alizotumia kubainisha sifa za muundo wa taarifa na sababu za upinduzi wa kimahali katika mawasiliano. Katika mbinu ya upimaji wa usahihi wa kisarufi, mtafiti aliandaa mwongozo wa upimaji wa usahihi wa kisarufi. Mwongozo huo ulitumika kupima tungo zenye upinduzi wa kimahali zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Katika mwongozo huo, mtafiti aliwaomba watoataarifa wawili wabainishe kama tungo hizo zina usahihi wa kisarufi au hazina usahihi wa kisarufi. Kwa kuwa watoataarifa hao walikuwa na sifa zilizolengwa, mbinu hii ilimwezesha mtafiti kupata tungo sahihi zenye upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili. Tungo hizo ndizo alizotumia kuchambua sifa za muundo wa taarifa na sababu za upinduzi wa kimahali katika mawasiliano. Katika mbinu ya usaili, mtafiti alifanya usaili nusu funge kwa watoataarifa wanane. Katika mbinu hii, mtafiti aliandaa mwongozo wa usaili wenye sehemu kuu mbili, yaani A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali yaliyolenga kupata data zinazohusu viambajengo gani vya tungo hizo vinatoa taarifa ya mada na vipi vinatoa taarifa ya fokasi kwa kuzingatia sifa za kimofosintaksia za viambajengo hivyo. Sehemu hii ilimsaidia mtafiti kubainisha sifa za muundo wa taarifa wa tungo zenye upinduzi wa kimahali ili kufikia lengo la kwanza la utafiti uliozaa makala haya. Sehemu B ilikuwa na pea 5 zenye sentensi mbilimbili, yaani sentensi (a) na (b). Katika kila pea, sentensi (a) ilikuwa tungo isiyo na upinduzi wa kimahali na sentensi (b) ilikuwa ni yenye upinduzi wa kimahali. Kisha mtafiti aliwaomba watoataarifa kueleza sababu za kutumia sentensi (b) na sio sentensi (a). Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kujua sababu za upinduzi wa kimahali katika mawasiliano ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Sababu hizi hazikuwekwa wazi na watafiti waliotangulia katika lugha ya Kiswahili (taz., kwa mfano, Mkude, 2005) au lugha nyingine za Kibantu (Salzman, 2004).

Aidha, baada ya kukusanya data, data hizo zilichambuliwa na kufasiriwa kwa kutumia misingi ya mkabala wa Sarufi Leksia Amilifu (Bresnan na Kanerva, 1970).

Mkabala huo pamoja na misingi yake umeelezwa katika sehemu inayofuata, yaani sehemu 3.0.

**3.0 Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu**

Sarufi Leksia Amilifu (kuanzia sasa SLA) ni nadharia iliyoasisiwa na Joan Bresnan na Ronald Kaplan mwishoni mwa miaka ya 1970. Nadharia hii inachanganua sentensi kwa kutumia taarifa za kileksika na uamilifu wa viambajengo vinavyounda sentensi inayohusika. Aidha, nadharia hii inahusisha matumizi ya mikabala mbalimbali katika uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi. Mikabala hiyo ni Mkabala wa Miundo ya Viambajengo (MMV), Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo (MUV), Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi (MVK) na Mkabala wa Muundo Taarifa (MMT). Kwa kuzingatia malengo ya makala haya, Mkabala wa Muundo wa Taarifa (MMT) umetumika katika uchambuzi na ufasiri wa data.

Mkabala wa Muundo wa Taarifa (MMT) ni mkabala unaohusu taarifa zinazowakilishwa na viambajengo vya sentensi katika mawasiliano. Kwa mujibu wa mkabala huu, kuna aina kuu mbili za taarifa, yaani mada na fokasi. Hivyo, mkabala huu unasaidia kubainisha viambajengo gani vinawakilisha taarifa ambayo ni mada na viambajengo gani vinawakilisha taarifa ambayo ni fokasi. Kuhusiana na muundo wa taarifa, Bresnan na Mchombo (1987) wameunda Nadharia ya Dhima za Kilongo (kuanzia sasa NDhK) ili kufafanua muundo wa taarifa katika tungo, yaani aina ya taarifa na sifa za kimofosintaksia zinazoambatana na viambajengo vinavyowakilisha taarifa hizo. Kwa mujibu wao, kiambajengo kinachowakilisha mada kina tabia mbalimbali kama ifuatavyo: ni kiima cha sentensi yenye mpangilio wa kawaida, kinaweza kurejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi cha urejeshi, kinaweza kuwakilishwa na kiwakilishi huru au tegemezi na wala hakiwezi kuulizwa au kuwakilishwa na neno ulizi katika nafasi yake. Kwa upande mwingine, kiambajengo kinachowakilisha taarifa ambayo ni fokasi kina tabia zifuatazo: kinaweza kuulizwa au kuwakilishwa na neno ulizi katika nafasi yake, kinaweza kuwekewa mkazo wa juu kuliko viambajengo vingine, hakiwezi kuwakilishwa na kiwakilishi huru au tegemezi na wala hakiwezi kurejeshwa na kuwakilishwa na kiwakilishi rejeshi katika kitenzi cha sentensi. Aidha, kuhusiana na fokasi, Salzman (2004: 91) anaeleza kamba maneno ulizi hubeba dhana ya fokasi, yaani taarifa mpya. Hii ni kwa sababu fokasi ni taarifa mpya na inayosisitizwa katika tungo. Kiulizi kinahusishwa na fokasi kwa sababu ni taarifa mpya ambayo haijulikani na mpokeaji.

Kwa kuzingatia sifa za mada na fokasi zilizoelezwa katika NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987), mkabala huu umetumika kubainisha sifa za muundo wa taarifa katika sentensi zenye upinduzi wa kimahali pamoja na sababu za upinduzi wa kimahali katika mawasiliano ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

## 4.0 Tungo zenye Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili

Kama ilivyo katika tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili (kwa mfano, Marten na van der Wal, 2014; Hassan, 2018 na Hassan, 2019), utafiti uliozaa makala haya pia umebaini kwamba lugha ya Kiswahili ina tungo zenye upinduzi wa kimahali. Kwa kuzingatia data zilizokusanywa na kufasiriwa kwa kutumia misingi ya SLA, hususani NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987), tungo hizo zina muundo wake wa taarifa. Pia, zinatokea kwa sababu mbalimbali katika mawasiliano. Kwa hiyo, sehemu hii inahusu uwasilishaji na ufafanuzi wa data kuhusu sifa za muundo wa taarifa na sababu za upinduzi wa kimahali katika mawasiliano ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Sehemu ndogo ya. 4.1 inahusu sifa za muundo wa taarifa wa tungo zenye upinduzi wa kimahali katika Kiswahili.

### 4.1 Sifa za Muundo wa Taarifa za Tungo zenye Upinduzi wa Kimahali

Sifa za Muundo wa taarifa unajumuisha aina za taarifa pamoja na sifa zake za kimofosintaksia. Data zinabainisha kwamba katika tungo zenye upinduzi wa kimahali kuna aina kuu mbili za taarifa. Taarifa hizo ni mada pamoja fokasi. Mfano Na. (2) unaonesha taarifa hizi mbili katika tungo yenye upinduzi wa kimahali za lugha ya Kiswahili:

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 (a) | ***Unguja*** | ***pa-*** | ***me-*** | ***ja-*** | ***a*** | ***wa-geni*** | |
| | kng16.Unguja | | kk16 | knj | ja | kt | kng2-geni |
| | 'Unguja pamejaa wageni.' | | | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (b) | Viambajengo | Unguja | pamejaa | wageni |
| | Aina ya Taarifa | Mada | Fokasi | |

Mfano Na. 2 (a) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali *Unguja pamejaa wageni*. Tungo hii ina viambajengo viwili, yaani *Unguja* pamoja *pamejaa wageni*. Mfano Na. 2 (b) unaonesha kwamba kiambajengo *Unguja* ni mada na kiambajengo *pamejaa wageni* ni fokasi. Kwa hiyo, ni wazi kwamba katika tungo yenye upinduzi wa kimahali kuna aina mbili za taarifa, yaani mada na fokasi. Viambajengo vinavyowakilisha mada na fokasi vina tabia mbalimbali za kimofosintaksia (Bresnan na Mchombo, 1987). Aina hizi za taarifa na sifa zake za kimofosintaksia zimefafanuliwa katika sehemu za 4.1.1 na 4.1.2.

#### 4.1.1 Mada

Mada, kwa mujibu wa Lambrecht (1994), ni kiambajengo dhanilizwa ambacho kinabeba taarifa ya zamani au kuukuu. Kwa kuzingatia fasili ya Lambrecht, katika makala haya, istilahi 'mada' imetumika kwa namna mbili. Mosi, mada ni taarifa ya zamani inayojulikana katika sentensi. Taarifa hii inajulikana kwa wote, yaani mtoaji na mpokeaji wa taarifa. Aidha, taarifa hii inajulikana na inaweza kukumbukwa na mpokeaji wa taarifa kwa sababu imetajwa katika tungo

zilizotangulia au imewasilishwa kama taarifa inayojulikana kwa kutumia mbinu za kiisimu. Pili, mada inaweza kufasiliwa kama taarifa inayoonesha kwamba sentensi inahusu nini. Kwa sababu hiyo, mada ni taarifa ambayo inapewa kipaumbele katika sentensi.

Kwa kuzingatia data za makala haya, katika tungo zenye upinduzi wa kimahali, mada ni kimahali ambacho kimepinduliwa. Mfano Na. 3 (b) unaonesha kwamba katika tungo yenye upinduzi wa kimahali, mada ni kimahali kilichopinduliwa:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | (a) *Maji* | *ya-* | *me-* | *ja-* | *a* | ***shimo-ni*** |
| | kng6.maji | kk6 | knj | mz | kt | kng5-ktm |

'Maji yamejaa shimoni.'

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (b) ***Shimo-ni*** | *m-* | *me-* | *ja-* | *a* | *maji* |
| kng5-ktm | kk16 | knj | mz | ktm | kng6.maji |

'Shimoni mmejaa maji.'

Mfano Na. 3 (b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili. Tungo hii ina vishiriki viwili ambavyo ni kimahali kilichopinduliwa na kithimu. Katika tungo hii, kimahali kilichopinduliwa ni *shimoni* na kithimu ni *maji*. Kwa hiyo, mada ni kimahali kilichopinduliwa *shimoni*. *Shimoni* ni mada kwa sababu ni kiambajengo kinachoonesha kwamba tungo nzima inaeleza kuhusu *shimoni* na sio viambajengo vingine.

Kwa kuzingatia misingi ya mkabala wa Sarufi Leksia Amilifu (Bresnan na Kaplan, 1982) ambao uliendelezwa katika Nadharia ya Dhima za Kilongo (NDhK) (Bresnan na Mchombo, 1987), katika tungo zenye upinduzi wa kimahali mada ni kimahali kilichopinduliwa kwa sababu ya sifa zifuatazo:

**(a) Kimahali Kilichopinduliwa ni Kiima**

Kwa kuzingatia data tulizozikusanya, kimahali kilichopinduliwa ni kiima. Kiima ni kiambajengo ambacho, katika mpangilio wa kawaida wa viambajengo vya sentensi za Kiswahili, kinatokea mwanzoni mwa sentensi, yaani kabla ya kitenzi. Pia, kiambajengo hicho ndicho kinachoukilia upatanishi wa kisarufi katika kitenzi (Keenan, 1976a; TUKI, 1990; van Valin, 2001: 33-59; na Mkude, 2005: 30). Kwa hiyo, katika sentensi zenye upinduzi wa kimahali, kimahali kilichopinduliwa ni kiima kwa sababu kinatokea mwanzoni mwa sentensi, yaani kabla ya kitenzi. Pia, kinaukilia upatanishi wa kisarufi katika kitenzi kwa kutumia viambishi vya upatanishi wa kiima vya ngeli ya ama 16 {*pa*-}, 17 {*ku*-} au 18 {*mu*-}. Kwa kuwa kimahali kilichopinduliwa ni kiima, basi kinatoa taarifa ambayo ni mada katika sentensi. Kwa mujibu wa NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987), kiambajengo kinachotoa taarifa ya mada, kwa kawaida, huwa ni kiima cha sentensi. Kiima kwa mujibu wa nadharia hii, hakihusishwi na dhima mahususi ya kisemantiki [-h] na wala hakina tabia za uyambwa [-y]. Kielelezo Na. 2 kinathibitisha hoja hii:

**Kielelezo Na. 2: Mada katika Tungo yenye Upinduzi wa Kimahali**
*Shimoni mmejaa maji.*

| | | | |
|---|---|---|---|
| Viambajengo | Shimoni | mmejaa | maji |
| ↓ | ↓ | ↓ | ↓ |
| Dhima za Kisarufi | Kiima | Kitenzi | Yambwa$_{\theta}$ |
| ↓ | ↓ | ↓ | ↓ |
| Sifa Bainifu | [-h, -y] | Kitenzi | [+h, +y] |
| ↓ | ↓ | ↓ | ↓ |
| Aina ya Taarifa | Mada | -------- | ---------- |

Kielelezo Na. 2 kinaonesha kwamba katika tungo yenye upinduzi wa kimahali, *shimoni mmejaa maji*., kimahali kilichopinduliwa *shimoni* ni kiima [-h, -y] ambacho pia kinatoa taarifa ambayo ni mada katika sentensi.

**(b) Kimahali Kilichopinduliwa Kinarejeshwa na Kuwakilishwa na Kiambishi cha Urejeshi**
Kiambishi cha urejeshi ni kiambishi kinachoambikwa ili kurejelea nomino kiima, yambwa au yambiwa katika sentensi. Kiambishi hiki kina muundo wa o-rejeshi kwa kuzingatia ngeli ya nomino inayorejeshwa. Aidha, kiambishi hiki kinaambikwa katika kishazi tegemezi bebwa cha urejeshi bainifu au si bainifu. Kiambishi hiki kina nafasi tatu za utokeaji wake. Nafasi hizo ni kabla ya mzizi wa kitenzi (mfano, *ana**ye**ingia*), baada ya kiambishi tamati cha kitenzi (mfano, *aingia**ye***) na baada ya *amba* (mfano, *amba**ye***).

Kwa kuzingatia data tulizozikusanya katika utafiti uliozaa makala haya, kimahali likichopinduliwa ni nomino ambayo inaweza kurejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi cha urejeshi katika kitenzi. Kwa hiyo, kwa kuzingatia NDhK (Brenan na Mchombo, 1987), kimahali kilichopinduliwa ni mada kwa sababu kinaweza kurejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi cha urejeshi kinachoambikwa kwenye kitenzi. Mfano Na. 4 (b) unaonesha urejeshaji wa kimahali kilichopinduliwa:

4 (a)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *sakafu-ni* | *pa-* | *me-* | *zaga-* | *a* | *wa-dudu* |
| kng9.sakafu-ktm | kk16 | knj | zaga | kt | kng2-dudu |

‘Sakafuni pamezagaa wadudu.’


(b)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ***Sakafu-ni*** | *pa-li-**po**-f-i-a* | *siafu* | *pa-me-zaga-a* | *wa-dudu* |
| kng9.sakafu-ktm | kk16-knj-krj16-mz-ktndea-kt | kng2.siafu | kng16-knj-zaga-kt | kng2-dudu |

‘Sakafuni palipofia siafu pamezagaa wadudu.’

Mfano Na. 4 (b) unaonesha kwamba kimahali kilichopinduliwa sakafuni kimerejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi cha urejeshi cha ngeli ya 16 {-*po*-}. Kiambishi hiki kimeambikwa kabla ya mzizi wa kitenzi cha kishazi tegemezi bebwa cha urejeshi *palipofia*. Kwa hiyo, ni wazi kwamba kimahali kilichopinduliwa ni mada katika sentensi. Kielelezo Na. 3 kinaonesha urejeshaji wa kimahali kilichopinduliwa kwa kuzingatia misingi ya SLA:

**Kielelezo Na. 3: Urejeshaji wa Kimahali Kilichopinduliwa**




Kielelezo Na. 3 kinaonesha kwamba kimahali kilichopinduliwa *sakafuni* kimeweza kurejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi cha urejeshi {-*po*-} ambacho kimeambikwa kabla ya mzizi wa kitenzi *palipofia* katika kishazi tegemezi bebwa cha urejeshaji bainifu *palipofia siafu*. Hivyo, katika tungo zenye upinduzi wa kimahali, mada ni kimahali kilichopinduliwa.

**(c) Kinahusishwa na Kipatanishi cha Kiima katika Kitenzi**

Kwa kuzingatia data tulizozikusanya, kimahali kilichopinduliwa kinahusishwa na kiambishi cha upatanishi wa kiima katika kitenzi. Kwa kuwa kinahusishwa na kiambishi cha upatanishi wa kiima, basi kinaweza kuwakilishwa na kiambishi hicho hata kama kimahali hicho hakijatajwa katika sentensi hiyohiyo au inayofuatia. Kwa mujibu wa NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987), kiambajengo kinachoweza kuwakilishwa na kiwakilishi huru au tegemezi (mfano, kiambishi cha uptanishi wa kiima) kinawakilisha taarifa ambayo ni mada. Kwa kuzingatia msingi huu, kimahali kilichopinduliwa katika tungo yenye upinduzi wa kimahali kinawakilisha taarifa ambayo ni mada. Mfano katika data Na. (5) unathibitisha hoja hii:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | (***Nyumba-ni*** *)* | ***ku-*** | *me-* | *ja-* | *a* | *wa-geni* |
| | kng9.nyumba-ktm | kk17 | knj | ja- | kt | kng2-geni |
| | 'Nyumbani kumejaa wageni.' | | | | | |

Mfano Na. 5 unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, kimahali kilichopinduliwa *nyumbani* kinaweza kuwakilishwa na kiambishi cha upatanishi wa kiima cha ngeli ya 17 {*ku-*} katika kitenzi *kumejaa*. Hivyo, kwa kuzingatia misingi ya NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987), kimahali kilichopinduliwa *nyumbani* katika tungo za Kiswahili zenye upinduzi wa kimahali kinatoa taarifa ambayo ni mada.

**(d) Kinaweza Kuwakilishwa na Kiwakilishi Huru katika Tungo**

Kwa kuzingatia data tulizozikusanya, kimahali kilichopinduliwa kinaweza kuhusishwa na kiwakilishi huru katika sentensi. Kiwakilishi huru ni neno linalosimama badala ya neno jingine katika sentensi. Kwa kuwa kimahali kinaweza kuwakilishwa na kiwakilishi huru, basi kinaweza kisitajwe katika sentensi na bado sentensi hiyo ikawa na maana ileile. Kwa mujibu wa NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987), kiambajengo kinachoweza kuwakilishwa na kiwakilishi huru kinawakilisha taarifa ambayo ni mada. Kwa kuzingatia msingi huu, kimahali kilichopinduliwa katika tungo yenye upinduzi wa kimahali kinawakilisha taarifa ambayo ni mada. Mifano katika data Na. (6) inathibitisha hoja hii:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6. | (a) ***Chuo-ni*** | | ***ku-*** | *me-* | *ene-* | *a* | *ugonjwa* |
| | kng7-uo-ktm | kk17 | knj | ene- | kt | kng14.ugonjwa | |
| | 'Chuoni kumeenea ugonjwa.' | | | | | | |
| | (b) ***Kule*** | ***ku-*** | *me-* | *ene-* | *a* | *ugonjwa* | |
| | Kule | kk17 | knj | ene- | kt | kng14.ugonjwa | |
| | 'Kule kumeenea ugonjwa.' | | | | | | |

Mfano katika data Na. 6 (a) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, kimahali kilichopinduliwa ni *chuoni*. Mfano wa 6 (b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali kilichopinduliwa *chuoni* ambacho kimewakilishwa na kiwakilishi huru *kule*. Hivyo, kwa kuzingatia misingi ya NDhK (Bresnan na

Mchombo, 1987), kimahali kilichopinduliwa *chuoni* katika tungo hii ya Kiswahili ni mada.

Kwa ujumla, katika tungo zenye upinduzi wa kimahali, kimahali ambacho kimepinduliwa ni mada. Kwa kuzingatia misingi ya NDhK (Bresnan na mchombo, 1987), kimahali hicho ni mada kwa sababu ni kiima, kinaweza kurejeshwa na kinahusishwa na kiambishi cha upatanishi wa kiima. Vilevile, kimahali hicho ni mada kwa sababu kinaweza kuwakilishwa na kiwakilishi huru na wala hakiwezi kuwakilishwa na neno ulizi na bado kikabaki kuwa mada. Aidha, ikumbukwe kwamba mada sio taarifa pekee inayowakilishwa katika tungo zenye upinduzi wa kimahali. Taarifa nyingine ni fokasi. Taarifa hii imefafanuliwa katika sehemu inayofuata, yaani 4.1.2.

**4.1.2 Fokasi**

Fokasi ni dhana inayofafanuliwa na wanaisimu mbalimbali. Mathalani, Lambrecht (1994) na Ndung'u (2015) wanaeleza kuwa fokasi ni kiambajengo ambacho kinatoa taarifa mpya katika tungo. Naye Halliday (1967) anaeleza kwamba fokasi ni taarifa ambayo inaulizwa kwa kutumia mfumo wa swali na jibu. Vilevile, fokasi ni taarifa ambayo inaweza kuashiriwa na kibainishi cha fokasi katika maelezo. Kwa kuzingatia fasili hizo za Halliday (1967), Lambrecht (1994) na Ndung'u (2015), katika makala haya, tumetumia dhana ya fokasi kwa maana ya taarifa mpya. Kwa mujibu wa Sarufi Leksia Amilifu (SLA), hususani misingi ya NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987) kiambajengo kinachowakilisha fokasi kina tabia zifuatazo: kinaweza kuulizwa au kuwakilishwa na neno ulizi katika nafasi yake, kinaweza kuwekewa mkazo wa juu kuliko viambajengo vingine, hakiwezi kuwakilishwa na kiwakilishi huru au tegemezi na wala hakiwezi kurejeshwa na kuwakilishwa na kiwakilishi rejeshi katika kitenzi cha sentensi. Katika makala haya, tumefasiri (tumefafanua) data kwa kuzingatia misingi ya NDhK kama ilivyoelezwa na Bresnan na Mchombo (1987) na kushadidiwa pia na wanaisimu wengine kama vile Salzman (2004).

Kwa kawaida, kuna aina tatu za fokasi kama inavyoelezwa na Lambrecht (1994). Aina ya kwanza ni fokasi kishiriki. Hii ni fokasi finyu na inahusisha kiambajengo chochote kimoja mahususi katika sentensi. Aina ya pili ni fokasi prediketa. Hii ni fokasi pana na inahusisha kitenzi pamoja na viambajengo kadhaa katika kirai kitenzi. Lengo la fokasi hii ni kutoa maelezo kuhusu mada. Aina ya tatu ni fokasi sentensi. Hii ni fokasi ambayo inahusisha sentensi nzima. Fokasi hii haina udhanilizo wowote na lengo lake ni kuarifu tukio. Licha ya kuwapo kwa aina tatu za fokasi, makala haya yamejikita katika kufafanua fokasi kishiriki, hususani tukijikita katika viambajengo vinavyohusika katika tungo zenye upinduzi wa kimahali. Mfano Na. 7 unaonesha fokasi kishiriki katika tungo:

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | (a) *M-ji-ni* | | *ku-* | *me-* | *ene-* | *a* | ***nini?*** |
| | kng3-ji-ktm | kk17 | knj | ene | kt | nini? | |
| | 'Mjini kumeenea nini?' | | | | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (b) *M-ji-ni* | | *ku-* | *me-* | *ene-* | *a* | ***habari*** |
| kng3-ji-ktm | kk17 | knj | ene | kt | kng9.habari | |

‘Mjini kumeenea habari.’

Mfano Na. 7 (a) unaonesha kuwa kuna taarifa mpya ambayo haijulikani katika tungo. Taarifa hii imewakilishwa na kiulizi *nini*. Mfano Na. 7 (b) unaonesha kuwa taarifa iliyoulizwa ni *habari*. Kwa hiyo, fokasi kishiriki katika tungo Na. 7 (b) ni *habari*.

Kwa kuzingatia data tulizozikusanya katika utafiti uliozaa makala haya, fokasi kishiriki katika tungo yenye upinduzi wa kimahali ni kithimu. Mfano Na. 8)unathibitisha hoja hii:

8

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) ***Mi-mea*** | *i-* | *me-* | *staw-* | *i* | *shamba-ni* |
| kng4-mea | kk4 | knj | mz | kt | kng5.shamba-ktm |

‘Mimea imestawi shambani.’

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (b) *Shamba-ni* | *ku-* | *me-* | *staw-* | *i* | ***mi-mea*** |
| kng5.shamba-ktm | kk16 | knj | mz | ktm | kng4-mea |

‘Shambani kumestawi mimea.’

Mfano Na. 8 (b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili. Tungo hii ina vishiriki viwili ambavyo ni kimahali kilichopinduliwa *shambani* na kithimu kilichopinduliwa *mimea*. Katika tungo hii, fokasi kishiriki ni kithimu kilichopinduliwa *mimea*. Kielelezo Na. 4 kinaonesha fokasi katika tungo yenye upinduzi wa kimahali:

**Kielelezo Na. 4: Fokasi katika Tungo yenye Upinduzi wa Kimahali**
*Shambani kumestawi mimea.*

| | | | |
|---|---|---|---|
| Viambajengo | Shambani | Kumestawi | Mimea |
| | ↓ | ↓ | ↓ |
| Dhima za Kisarufi | Kiima | Kitenzi | $Yambwa_{\theta}$ |
| | ↓ | ↓ | ↓ |
| Sifa Bainifu | [-h, -y] | Kitenzi | [+h, +y] |
| | ↓ | ↓ | ↓ |
| Aina ya Taarifa --------- | -------- | Fokasi Kishiriki | |

Kielelezo Na. 4 kinaonesha kwamba katika tungo yenye upinduzi wa kimahali, *Shambani kumestawi mimea*., kithimu kilichopinduliwa *mimea* ni $yambwa_{\theta}$ [+h, +y] ambacho pia kinatoa taarifa ambayo ni fokasi katika sentensi.

Kwa kuzingatia misingi ya Mkabala wa Sarufi Leksia Amilifu (Bresnan na Kaplan, 1982) ambao uliendelezwa katika NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987), katika

tungo zenye upinduzi wa kimahali, fokasi kishiriki ni kithimu kilichopinduliwa. Kithimu kilichopinduliwa ni fokasi kishiriki kwa sababu ya sifa zifuatazo:

**(a) Kinaweza Kuulizwa na Kuwakilishwa na Neno Ulizi katika Sentensi**

Maneno ulizi ni yale yanayowakilisha taarifa mpya ambayo haijulikani katika tungo. Maneno haya yakitumika katika tungo zenye upinduzi wa kimahali, basi yanawakilisha taarifa mpya au inayosisitizwa katika tungo. Katika tungo zenye upinduzi wa kimahali, kithimu kilichopinduliwa kinaweza kuwakilishwa na neno ulizi. Mfano Na. 9 unathibitisha hoja hii:

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 9 | (a) *Ukuta-ni* | *pa-* | *me-* | *pak-* | *w-* | *a* | ***rangi*** |
| | kng9.ukuta-ktm | kk16 | knj | mz | ktndw | kt | kng9.rangi |
| | 'Ukutani pamepakwa rangi.' | | | | | | |
| | (b) *Ukuta-ni* | *pa-* | *me-* | *pak-* | *w-* | *a* | ***nini**?* |
| | kng9.ukuta-ktm | kk16 | knj | mz | ktndw | kt | kng9.rangi |
| | 'Ukutani pamepakwa rangi.' | | | | | | |

Mfano Na. 9 (b) unaonesha kwamba neno ulizi limewakilisha taarifa kuhusu kithimu *rangi*. Kwa mujibu wa NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987), kiambajengo kinachowakilisha taarifa ambayo ni fokasi kinaweza kuwakilishwa na neno ulizi. Kwa hiyo, ni wazi kwamba kithimu ambacho kimepinduliwa ni fokasi katika tungo yenye upinduzi wa kimahali.

**(b) Kinaweza Kuulizwa kwa Kutumia Maswali ya Ndiyo/Hapana**

Maswali ya *ndiyo* au *hapana* yakitumika yanalenga kupata jibu linalorejelea kiambajengo cha mwisho baada ya kitenzi katika sentensi. Ikumbukwe kwamba kiambajengo kinachoulizwa katika tungo ni fokasi. Katika tungo zenye upinduzi wa kimahali, kiambajengo kinachotokea baada ya kitenzi ni kithimu kilichopinduliwa. Kwa hiyo, kulingana na data zilizokusanywa, jibu la swali la ndiyo/hapana katika tungo zenye upinduzi wa kimahali hurejelea kithimu kilichopinduliwa ambacho kinatokea mwishoni mwa sentensi, yaani baada ya kitenzi. Kwa hiyo, katika tungo zenye upinduzi wa kimahali, fokasi ni kithimu kilichopinduliwa. Mfano Na. 10 unathibitisha hoja hii:

10 (a) *Ki-tanda-ni* *pa-me-tandik-w-a* *shuka?*
kng7-tanda-ktm kk16-tmlf-mz-ktndw-kt kng9.shuka?
'Kitandani pametandikwa shuka?'

(b) *Ndiyo, ki-tanda-ni* *pa-me-tandik-w-a* *shuka.*
Ndiyo, kng7-tanda-ktm kk16-tmlf-mz-ktndw-kt kng9.shuka.
'Ndiyo, kitandani pametandikwa shuka (Na siyo kitunkingine).'

Mfano wa 10 (a) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali iliyo na muundo wa tungo ya swali la ndiyo/hapana. Mfano wa 10 (b) unaonesha kwamba jibu la swali hilo linarejelea kiambajengo cha mwisho katika tungo hii na kiambajengo hicho ni

kithimu *shuka*. Kwa hiyo, katika tungo zenye upinduzi wa kimahali za lugha ya Kiswahili, fokasi kishiriki ni kithimu kilichopinduliwa.

**(c) Hakiwezi Kurejelewa/Kuwakilishwa na Kiambishi Yambwa**

Kiambishi yambwa ni kiambishi ambacho kinarejelea nomino ambayo ina uamilifu wa yambwa katika tungo. Kwa mujibu wa data tulizozikusanya katika utafiti uliozaa makala haya, kithimu ambacho hakijapinduliwa licha ya kuwa nomino, hakiwezi kurejelewa wala kuwakilishwa na kiambishi yambwa katika kitenzi. Hii ni kwa sababu kiambishi yambwa kinarejelea taarifa ambayo inajulikana. Kwa upande mwingine, fokasi ni taarifa mpya ambayo haijulikani. Kwa hiyo, kuambika kiambaishi yambwa katika kitenzi kunazalisha tungo isiyo sahihi kisarufi. Mfano Na. 11 unathibitisha hoja hii:

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 11 | (a) *Kiwanja-ni* | *pa-* | *me-* | *me-* | *a* | ***nyasi*** | |
| | kng7-wanja-ktm | kk16 | knj | mz | kt | kng10.nyasi | |
| | (b) **Kiwanja-nipa-* | ****zi-*** | *me-* | *me-* | *a* | ***nyasi*** | |
| | kng7-wanja-ktm | kk16 | ky10 | knj | mz | kt | kng10.nyasi |
| | (c) **Kiwanja-nipa-* | ****zi-*** | *me-* | *me-* | *a* | | |
| | kng7-wanja-ktm | kk16 | ky10 | knj | mz | kt | |

(a) ‘Kiwanjani pamemea nyasi.’

(b) ‘Kiwanjani pamezimea nyasi.’

(c) ‘Kiwanjani pamemea.’

Mfano Na. 11 (a) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili. Katika tungo hii, kithimu ni kiambajengo *nyasi*. Mfano Na. 11 (b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali ambayo haikubaliki katika lugha ya Kiswahili. Tungo hii haikubaliki kwa sababu kithimu kilichopinduliwa *nyasi* kimerejelewa na kiambishi yambwa katika kitenzi **pamezimea*. Mfano Na. 11 (c) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali ambayo haikubaliki katika lugha ya Kiswahili. Tungo hii haikubaliki kwa sababu kithimu kilichopinduliwa *nyasi*, kimewakilishwa na kiambishi yambwa katika kitenzi **pamezimea*. Tungo hizi hazikubaliki kwa sababu zinakiuka misingi ya NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987). Kwa mujibu wa nadharia hii, fokasi ni taarifa ambayo haiwezi kuwakilishwa na kiambishi cha yambwa ambacho kinahusiana na taarifa ambayo inajulikana katika tungo. Kwa hiyo, ni wazi kwamba katika tungo zenye upinduzi wa kiamhali, fokasi kishiriki ni kithimu ambacho kimepinduliwa.

**(d) Hakiwezi kuwa Kiima cha Sentensi Tendwa**

Sentensi tendwa ni sentensi ambayo mtendwa hupandishwa hadhi na kutokea katika nafasi ya kiima, na kwa upande mwingine, mtenda hushushwa hadhi na kuwekwa baada ya kitenzi. Kwa kuzingatia data tulizozikusanya katika utafiti uliozaa makala haya, katika tungo yenye upinduzi wa kimahali, kithimu ambacho kimepinduliwa hakiwezi kuwa kiima cha sentensi tendwa. Hakiwezi kuwa kiima cha sentensi

tendwa kwa sababu kiima ni taarifa ambayo inayojulikana na inadokeza tungo inahusu nini (mada). Kwa kuwa kithimu kilichopinduliwa hakidokezi taarifa inayojulikana, hakiwezi kulazimishwa na kuwa kiima cha sentensi tendwa. Kufanya hivyo ni kuzalisha tungo isiyokubalika, kama inavyoonekana katika mfano Na. (12):

12 (a) *Shimo-ni* *m-* *me-* *ingi-* *a* *nyoka*
kng5.shimo-ktm kk18 knj ingi kt kng1.nyoka
'Shimoni mmeingia nyoka.'
(b) **Nyoka* *a-* *me-* *ingil-* *w-* *a* *na* *shimo-ni*
kng1.nyoka kk1 knj ingil ktndw kt na kng5.shimo-ktm
'Nyoka ameingiliwa na shimoni.'

Mfano Na. 12 (a) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili. Katika tungo hii, kithimu ambacho kimepinduliwa ni *nyoka*. Mfano Na. 12 (b) unaonesha tungo yenye upiduzi wa kimahali ambayo haikubaliki katika lugha ya Kiswahili. Tungo hii haikubaliki kwa sababu kithimu *nyoka* hakiwezi kuwa kiima cha sentensi tendwa. Hakiwezi kuwa kiima cha sentensi tendwa kwa sababu kwa mujibu wa NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987) kithimu *nyoka* kinadokeza taarifa mpya na siyo taarifa ya zamani (mada). Kwa hiyo, ni wazi kwamba katika tungo zenye upinduzi wa kimahali, kithimu kilichopinduliwa ni fokasi kishiriki.

Kwa hiyo, katika tungo zenye upinduzi wa kimahali, kithimu ambacho kimepinduliwa ni fokasi kishiriki. Kwa kuzingatia misingi ya NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987), kithimu hicho ni fokasi kwa sababu zifuatazo: kinaweza kuulizwa kwa kutumia maneno ulizi katika nafasi yake, kinaweza kuulizwa kwa kutumia maswali ya ndiyo/hapana, hakiwezi kurejelewa au kuwakilishwa na kiambishi yambwa na hakiwezi kuwa kiima cha sentensi tendwa.

Kwa ujumla, sehemu ya 4.1 imebainisha na kufafanua sifa za muundo wa taarifa za tungo zenye upinduzi wa kimahali kwa kuzingatia misingi ya NDhK (Bresnan na Mchombo, 1987). Kwa mujibu wa misingi hiyo, kimahali kilichopinduliwa ni mada na kithimu kilichopinduliwa ni fokasi kishiriki. Aidha, muundo huu wa taarifa una matumizi yake katika mawasiliano ya watumiaji wa lugha ya kawaida. Kwa hiyo, sehemu inayofuata inahusu sababu za upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili.

**4.2 Sababu za Upinduzi wa Kimahali katika Mawasiliano**

Utafiti uliozaa makala haya umebaini kwamba, upinduzi wa kimahali hautokei kiholela tu. Kwa mujibu wa data zilizokusanywa, upinduzi wa kimahali unatokea kwa sababu mbalimbali katika mawasiliano ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

Sababu hizo zinalenga kufanikisha mawasiliano baina ya mtoaji na mpokeaji wa taarifa. Sababu hizo ni hizi zifuatazo:

**(a) Umadaishaji wa Kimahali**

Umadaishaji wa kimahali ni mchakato wa kisintaksia ambao kwao kimahali kinapandishwa hadhi na kuwa mada katika sentensi. Kimahali hicho kinafanywa kuwa taarifa ambayo inajulikana na wote wawili, yaani mtoaji na mpokeaji wa taarifa. Wakati mwingine, kimahali kinapandishwa hadhi na kufanywa kuwa mada iwapo kinahusu taarifa ya zamani ambayo ilikwishatajwa hapo awali. Katika mawasiliano, umadaishaji wa kimahali unasaidia kuweka wazi kwamba taarifa inayojulikana na mtoaji na mpokeaji taarifa ni kuhusu mahali. Pia, inasaidia kudokeza kwamba taarifa hii ni ya zamani kwa kuwa ilikwishatajwa katika tungo zilizotangulia. Ili kufanya mambo yote mawili, kimahali kinapandishwa hadhi na kutokea mwanzoni mwa sentensi, yaani kabla ya kitenzi.

Kulingana na data zilizokusanywa, imebainika kwamba upinduzi wa kimahali unatokea ili kumadaisha kimahali. Umuhimu wa umadaishaji huo ni kuweka wazi kwamba ujumbe ambao mtoaji wa taarifa anadhani kwamba mpokeaji anaufahamu pia ni kimahali ambacho kimepinduliwa. Pia, kuweka wazi kwamba ujumbe ambao ulikwishatajwa hapo awali ni kuhusu kimahali kilichopinduliwa. Lengo la kufanya mambo haya yote mawili ni kufanikisha mawasiliano yanayofanyika. Mfano Na. 13 unathibitisha hoja hii:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 13 | (a) *Nyasi* | *zi-* | *me-* | *ot-* | *a* | *ki-wanja-ni* |
| | kng10.nyasi | kk10 | knj | mz | kt | kng7-wanja-ktm |
| | ‘Nyasi zimeota kiwanjani’. | | | | | |
| | (b) ***ki-wanja-ni*** | *pa-* | *me-* | *ot-* | *a* | *nyasi* |
| | kng7-wanja-ktm | kk16 | knj | mz | kt | kng10.nyasi |
| | ‘Kiwanjani pameota nyasi.’ | | | | | |

Mfano Na. 13 (a) unaonesha tungo isiyo na upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, taarifa ambayo inajulikana na wote ni kuhusu kithimu *nyasi*. Kwa upande mwingine, mfano Na. 13 (b) unahusu tungo yenye upinduzi wa kimahali. Tungo hii inahusu kimahali *kiwanjani*. Katika tungo hii, taarifa inayojulikana na wote ni kuhusu mahali kiwanjani. Kwa hiyo, mfano Na. 13 (b) unadhihirisha sababu ya upinduzi wa kimahali kwamba ni kukifanya kimahali kuwa taarifa inayojulikana na wote, yaani mtoaji na mpokeaji wa taarifa.

Kwa upande mwingine, mfano Na. 14 unaonesha kwamba upinduzi wa kimahali umetokea ili kuonesha kwamba taarifa kuhusu kimahali kiwanjani ilikwishatajwa awali:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 14 | (a) *Nyoka* | *a-* | *me-* | *jifich-* | *a* | ***ki-wanja-ni*** |
| | kng1.nyoka | kk10 | knj | mz | kt | kng7-wanja-ktm |

'Nyoka amejificha kiwanjani.'

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (b) ***ki-wanja-ni*** | *pa-* | *me-* | *ot-* | *a* | *nyasi* |
| kng7-wanja-ktm | kk16 | knj | mz | kt | kng10.nyasi |

'Kiwanjani pameota nyasi.'

Mfano Na. 14 (a) unaonesha tungo ambayo imetaja mahali alipojificha nyoka kwamba ni kiwanjani. Mfano Na. 14 (b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, kimahali kimefanywa kuwa mada kwa sababu ni taarifa ambayo imekwishatajwa katika mfano Na. 14 (a). Kwa hiyo, ni kweli kwamba upinduzi wa kimahali unatokea ili kumadaisha kimahali kuwa kama taarifa inayojulikana na wote, yaani mtoaji na mpokeaji wa taarifa. Pia, kinafanywa kuwa mada kama taarifa ambayo ilikwishatajwa awali.

**(b) Ufokalishaji wa Kithimu**

Ufokalishaji wa kithimu ni mchakato ambao kwao kithimu kinafanywa kuwa kama taarifa mpya katika tungo. Kinafanywa kuwa taarifa mpya ambayo mtoaji wa taarifa anadhani kwamba mpokeaji haifahamu. Pia, kinafanywa kuwa taarifa mpya kwa sababu ndiyo taarifa inayosisitizwa katika tungo. Lengo la kukifanya kithimu kilichopinduliwa kuwa taarifa mpya au inayosisitizwa ni kufanikisha mawasiliano yanayofanyika. Mifano katika data Na. 15 inathibitisha hoja hii:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 15 | (a) ***Wa-geni*** | *wa-* | *me-* | *ja-* | *a* | *Bunge-ni* |
| | kng2-geni | kk2 | knj | mz | kt | kng5.Bunge-ktm |

'Wageni wamejaa Bungeni.'

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (b) *Bunge-ni* | *mu-* | *me-* | *ja-* | *a* | ***wa-geni*** |
| kng5.Bunge-ktm | kk18 | knj | mz | kt | kng2-geni |

'Bungeni mumejaa wageni.'

Mfano Na. 15 (a) unaonesha tungo isiyokuwa na upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, kithimu *wageni* kinawakilisha taarifa ambayo inajulikana, yaani mada. Mfano Na. 15 (b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali. Kithimu *wageni* katika tungo hii kinawakilisha taarifa mpya ambayo msemaji anadhani kwamba mpokeaji wake wa taarifa haifahamu. Kwa hiyo, upinduzi wa kimahali unatokea ili kufokalisha kithimu, yaani kukifanya kuwa fokasi katika sentensi.

**(c) Kufanya Ufokalishaji Linganuzi wa Kithimu**

Ufokalishaji linganuzi ni mchakato wa kisintaksia ambao kwao kiambajengo kinachowakilisha taarifa mpya, yaani fokasi kinatofautishwa na kiambajengo kingine ambacho kinaweza kuwakilisha taarifa kama hiyohiyo. Kulingana na data zilizokusanywa katika utafiti uliozaa makala haya, upinduzi wa kimahali unafanya pia ufokalishaji linganuzi kama inavyoonekana katika mifano iliyomo katika data Na. (16):

16( a)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ***Malaria*** | *i-* | *me-* | *ene-* | *a* | *Dodoma* |
| Kng9.Malaria | kk16 | knj | ene | kt | kng16.Dodoma |

'Malaria imeenea Dodoma.'

(b)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *Dodoma* | *pa-* | *me-* | *ene-* | *a* | ***malaria*** |
| Kng16.Dodomakk16 | knj | ene | kt | kng14.malaria | |

'Dodoma pameenea malaria.'

(c)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *Dodoma* | *pa-* | *me-* | *ene-* | *a* | ***malaria (sio kipindupindu)*** |
| Kng16.Dodomakk16 | knj | ene | kt | kng14.malaria (sio kipindupindu) | |

'Dodoma pameenea malaria (sio kipindupindu)'.

Mfano Na. 16 (a) unaonesha tungo isiyo na upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, kithimu *malaria* kinawakilisha taarifa ambayo ni mada. Mfano Na. 16 (b) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, kithimu *malaria* kinawakilisha taarifa mpya. Hata hivyo, taarifa hii inaweza kuchanganywa na taarifa nyingine kama vile *kipindupindu*. Mfano Na. 16 (c) unaonesha tungo yenye upinduzi wa kimahali. Katika tungo hii, taarifa mpya ni *malaria*. Taarifa hii mpya imeweza kutofautishwa na taarifa nyingine ambayo ni *kipindupindu*. Kwa hiyo, ni wazi kwamba upinduzi wa kimahali katika lugha ya Kiswahili unatokea ili kufanya ufokalishaji linganuzi wa kithimu. Lengo la kufanya hivi ni kufanikisha mawasiliano baina ya mtoaji na mpokeaji wa ujumbe.

Kwa ujumla, katika sehemu hii tumefafanua sababu za upinduzi wa kimahali. Kwa kuzingatia data, tumefafanua kwamba tungo zenye upinduzi wa kimahali zinatumika ili kufanya umadaishaji kimahali, kufanya ufokalishaji wa kithimu pamoja na kufanya ufokalishaji linganuzi wa kithimu. Kwa kuzingatia sababu hizi, ni wazi kwamba tungo hizi zina lengo kuu la kufanikisha mawasiliano yanayofanyika miongoni mwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

## 5.0 Hitimisho

Makala haya yameweka wazi kwamba tungo zenye upinduzi wa kimahali zinakiuka uhusiano uliopo baina ya udarajia wa dhima za kisemantiki na za kisarufi za viambajengo vya sentensi. Katika tungo hizi, kimahali ambacho kipo katika nafasi ya chini ya udarajia kinapandishwa hadhi na kuwa kiima cha sentensi hata kama katika tungo kuna kithimu au mtenda. Licha ya kufanyika kwa tafiti mbalimbali, na kisha kufafanua masuala ya msingi kama vile aina za tungo zenye upinduzi wa kimahali, vitenzi vinavyoruhusu na vile visivyoruhusu utokeaji wa tungo hizo, vimahali vinavyoweza kupinduliwa na vile visivyoweza kupinduliwa, dhima za kisarufi za viambajengo vinavyohusika na kadhalika; tafiti zilizotangulia hazikuweka wazi sifa za muundo wa taarifa za tungo zenye upinduzi wa kimahali pamoja na matumizi yake katika mawasiliano baina ya wanalugha. Hivyo, kuhusu sifa za muundo wa taarifa, makala yamebainisha kwamba katika tungo hizi mada ni kimahali kilichopinduliwa na fokasi kishiriki ni kithimu kilichopinduliwa. Kimahali ni mada kwa sababu ni kiima cha sentensi; kinaweza kurejeshwa na kuwakilishwa

na kiambishi rejeshi. Pia, kinahusishwa na kiambishi cha upatanishi wa kiima; na kinaweza kuwakilishwa na viwakilishi huru na hakiwezi kuulizwa na kuwakilishwa na kiulizi katika nafasi yake. Kwa upande mwingine, makala yameeleza kwamba kithimu kilichopinduliwa ni fokasi kwa sababu kinaweza kuulizwa na kuwakilishwa na maneno ulizi katika nafasi yake, kinaweza kuulizwa kwa kutumia maswali ya ndiyo/hapana, hakiwezi kuwakilishwa na kiambishi yambwa katika kitenzi na pia hakiwezi kuwa kiima cha sentensi tendwa. Aidha, kuhusu sababu za upinduzi wa kimahali, makala yameeleza kwamba upinduzi wa kimahali unatokea ili kufanya umadaishaji wa kimahali, ufokalishaji wa kithimu na ufokalishaji linganuzi wa kithimu. Kutokana na matokeo haya, makala yanahitimisha kwamba upinduzi wa kimahali hautokei kiholela bali unatokea ili kutengeneza sifa za muundo wake wa taarifa kwa lengo la kukidhi dhima kuu ya mawasiliano yanayofanyika.

**Marejeleo**

Ashton, E. O. (1944). *Swahili Grammar Including Intonation*. UK: Longman Group Ltd.

Baker, M. C. (1989). "Object Sharing and Projection in Serial Verb Constructions". *Linguistic Inquiry*, Juz. 20: 513 - 553.

Bresnan, J. na Kaplan, R. M. (1982). "Lexical-function Grammar: A Formal System for Grammatical Representation". Katika J. Bresnan (Mh.) *The Mental Representation of Grammatical Relations*. Cambridge: The MIT Press. kur.173-281.

Bresnan, J. na Kanerva, J. M. (1989). "Locative Inversion in Chichewa: A Case Study of Factorization in Grammar". *Linguistic Inquiry*, Juz. 20: 1- 50.

Bresnan, J. na Mchombo, S. A. (1987). "Topic, Pronoun and Agreemant in Chichewa". *Language*, Juz. 63: 741 - 782.

Buel, L. (2007). "Semantic and Formal Locatives: Implications for the Bantu Locative Inversion Typology". *SOAS Working Papers in Linguistics*, Juz. 15: 105 - 120.

Creissels, D. (2011) "Tswana Locatives and their Status in Inversion Construction". *Africana Linguistica*, Juz. 17: 33 - 52.

Demuth, K. na Mmusi, S. (1997). "Presentational Focus and Thematic Structure in Comparative Bantu". *Journal of African Languages and Linguistics*, Juz. 18: 1-19.

Diercks, M. (2009). "The Morphostyntax of Lubukusu Locative Inversion and Parameterization of Agreement". *Lingua*, Juz. 121: 702 - 720.

Dowty, D. (1991). "Thematic Proto-roles and Argument Selection". *Language*, Juz. 67(3): 547 - 619.

Halliday, M. A. K. (1967). "Notes on Transitivity and Theme in English". *Journal of Linguistics, Juz.* 3: 37 - 245.

Hassan, F. (2018). "Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili". *KIOO CHA LUGHA*, Juz. 16:165- 188.

Hassan, F. (2019). *Uchanganuzi wa Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hassan, F. (2019). "Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili: Dhima za Kisarufi na Sifa za Kimofosintaksia za Viambajengo Vinavyohusika". *KISWAHILI*, Juz. 82: 14- 43.

Her, O. (2003). "Chinese Inversion Constructions within a Simplified Lexical Mapping Theory". *Journal of Chinese Linguistics*, Juz. 6: 1 - 31.

Her, O. (2006). "Optimality-Theoretic, Lexical Mapping Theory: A Case Study of Locative Inversion". *International Journal of Technology and Human Interaction*, Juz. 2: 67 - 94.

Keenan, E. L. (1976). "Towards a Universal Definition of Subject". Katika C. N. Li (Mh.) *Subject and Topic*. New York: Academic Press. kur. 303 - 333

Khamis, M. A. (2008). *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: TUKI.

Krifka, M. (1959). "Swahili". Katika J. Joachim na T. Vennemann (Wah.) *Syntax*. Berlin/New York: De Gruyter. kur. 1397-1418.

Lambrecht, K. (1994). *Information Structure and Sentence Form: Topic, Focus, and Mental Representation of Discourse Referents*. Cambridge: Cambridge University Press.

Marten, L. (2006). "Locative Inversion in Otjiherero: More on Morphostntactic Variation in Bantu". *ZAS Papers in African Linguistics*, Juz. 43: 97 - 122.

Marten, L. (2013). "Structure and Interpretation in Swahili Existential Constructions". *Rivista di Linguistica*, Juz. 25 (1): 45 - 73.

Marten, L. na Van der Wal, J. (2014). "A Typology of Bantu Subject Inversion". *Linguistic Variation*, Juz. 14 (2): 318 - 368.

Mkude, D. J. (2005). *The Passive Constructions in Swahili*. Tokyo: Research Institute for Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).

Ndung'u, N. M. (2015). "Information Structure in Kiswahili". *International Journal of Education and Research*, Juz. 3 (3): 309 – 320.

Salzmann, M. D. (2004). *Theoretical Approaches to Locative Inversion*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Zurich: Chuo Kikuu cha Zurich.

TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Van Vallin, R. (2001). "Grammatical Relations in Ergative Languages". *Studies in Languages*, Juz. 5: 361-394.

Vitale, A. (1977). *Swahili Syntax*. Dordrecht: Foris Publications.

Whiteley, W. H. (1968). *Some Problems of Transitivity in Swahili*. London: School of Oriental and African Studies, University of London.

Zeller, J. (2013). "Locative Inversion in Bantu and Predication". *Linguistics*, Juz. 51 (6): 1107 - 1146.

**Alama na Vifupisho Vilivyotumika**

| | | |
|---|---|---|
| +h | = | Kinahusishwa na Dhima ya Kisemantiki Mahususi |
| -h | = | Hakihusishwi na Dhima ya Kisemantiki Mahususi. |
| kk | = | Kipatanishi cha Kiima |
| kng | = | Kiambishi cha Ngeli |
| knj | = | Kiambishi cha Njeo |
| krj | = | Kiambishi cha Urejeshi |
| kt | = | Kiabishi cha Tamati |
| ktm | = | Kiambishi Tamati cha Mahali |
| ktndea | = | Kiambishi cha Utendea |
| ktndw | = | Kiambishi ya Utendwa |
| ky | = | Kiambishi cha Yambwa |
| MMT | = | Mkabala wa Muundo Taarifa |
| MMV | = | Mkabala wa Miundo ya Viambajengo |
| MUV | = | Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo |
| MVK | = | Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi |
| mz | = | Mzizi |
| NDhK | = | Nadharia ya Dhima za Kilongo |
| SLA | = | Sarufi Leksia Amilifu |
| +y | = | Kina Tabia za Yambwa |
| -y | = | Hakina Tabia za Yambwa |
| * | = | Isiyosahihi Kisarufi |